Tuzungumuze

Akina dada na kaka wetu si mujiheshimu !

Ngoma ikilia sana haikawi kupasuka na ivumayo haidumu hunena mzee mungwana.

Kulingana na maneno hayo nimejiruhusu kushika tena kalamu yangu kwa kuwajulisha jambo moja linalotusonga moyoni wakati ninajitembeza mikoani. Jambo hilo laling̃ana na mwenendo mbaya wa akina dada na kaka zetu wasioheshimu siku hizi wazazi wao hata kidogo.

Mara nyingi twawaona dada na kaka hao wakitangatanga barabarani wasijue wakwendako.

hilo laonekana hasa wakati huu wa mafungo. Wale wanokuwa bado masomoni wajielekeza huko bila nia yoyote ya kujielimisha. Wadanganya wazazi eti wakwenda kuchuma elimu shuleni japokuwa shabaha yao maalum ni kujigeuza malaya.

Kwa ngambo ya wadada, hawa hujigeuza wanawake wa furaha wa mabwana wenye feza na kwa ngambo ya wakaka, hawa hujigeuza nao wale tunaozoea kuita hapa kwetu wa "jeunes premiers"ama" petits poussins" kwa kuwafurahisha ao kuwategemea akina mama wenyi pato lakutoshelea. Akina mama hao wana umri wa mama zao ao ule wa mamakuu zao.

Dada na kaka hao wajielekeza kanisani si kwa kuomba Mwenyezi Mola (Mungu), bali kwa kuonyesha mavazi wanayovaa na hali ya mwili wao baada ya kuunguza nywele zao na kutumia sabuni na dawa nyingine za kujichubuwa ngozi na kugeuka kama nguruwe zilizomwangiwa maji ya moto. Wakienda sokoni, dukani, kwenye michezo, sinema na penginepo, wanachekelea akina mama ao baba wasio na mavazi kama yao ama feza nyingi kwa kununua vyakula ama vitu vyenyi samani kubwa wanavyotia katika vikapo ao mikoba yenyi kuonya vyote vilivyomo.

Haya ya jamaa zao ndiyo furaha kwao. Wadada wa mtindo huo, wakisha kubeba mimba, kwa mfano, hawaoni hata woga wowote wa kutoa mimba hiyo ijapokuwa wanajua wazi kama ni hatari kabisa na ni hasara kwa afia yao. Kwa ngambo ingine sijui tuseme je juu ya wale akina dada wanaotupa watoto waliowazaa katika vyoo ao katika yalala na mifereji. Wavulana baada ya kuwabebesha wabinti mimba ingawa hawa na ginsi ya kuwatunza wala nyumba kwa kulala, hawa huwatupilia kwa wazazi wao ingawa hawana pato lakutoshelea kwa kuwatunza na kutunza bibi na mtoto. Ukiuliza akina dada kisa kilichowatuma kutenda hivyo, wao hujibu kuwa wadanganywa na rafiki zao wa kiume. Vijana hao wa waume hujisemea kuwa dada hao wamewasingizia uwongo kwani mzigo huo waliupata baada ya kutembea kisirisiri popote mikoani na wa "baba sukari" walio na pesa nyingi. Kwa kutowapatisha wababa hao haya mbele ya wake zao, dada zet huwasingizia sasa wavulana eti ni wao ndio waliowabebesha mimba.

Vitendo munavyovifany ni vya haya kabisa kwan vyazaraulisha wazazi wenu. Ni lazima sana mujiulize vizuri juu y vitendo vyenu na mufany bidii ya kubadilish mwendo mukiheshimu wazazi waliojitolea kwen bila kuwaomba lolote Yaonekana wazi kama hamutegemee sheria ama kanuni yoyote inayoelekea maisha.

Basi akina dada na kaka mujiheshimu kwani mungwana husema : Taratibu ndiyo mwendo na mwendo na tamaa yaua mtu pia njia mbili zilimshinda mzee fisi.

Bisimwa L.B. Tserou

Kivu ya Kusini

Padri Gapangwa atajwa Askofu mpya wa Diosezi ya Uvira

Mnamo tarehe 27 Julay 1985, Baba mtakatifu wa Roma, Papa Yoane-Paulo wa pili alimtaja padri Gapangwa kama vile askofu mpya wa diosezi katoliki ya Uvira. Habari hiyo ilitolewa kwa waumini wa dini katoliki na akina arkiaskofu Mulindwa Mutabesha mnamo tarehe 28 Julay wakati ya misa ya upadrisho iliyosomwa kunako uwanja Mobutu mtaani Kadutu, mjini Bukavu.

Wasomaji wetu wataelewa kuwa padri Gapangwa ndiye askofu wa tatu wa diosezi ya Uvira. Tangu Julay 1984 mpaka kutajwa kwake kama askofu mheshimiwa huyo alikuwa akihusika na uongozi wa diosezi ya hiyo. Aliachiwa madaraka hayo na akina askofu Dheju, aliyemkomboa askofu wa kwanza Catarzi mbele arejee kuiongoza diosezi ya Bunia katika jimbo la Zaïre ya Juu (Haut-Zaïre).

Padri Gapangwa ndiye askofu wa kwanza mzaliwa wa diosezi hiyo ya Uvira.

Ni mmoja kati ya mapadri Mutimanwa, Mugandja na Gapangwa ndiye alikuwa akizaniwa kupewa madaraka hayo.

Furaha kubwa pia kwa kanisa katoliki jimboni na hasa kwa diosezi ya Bukavu ni kuona ilijipatia tena mapadri wengine wawili wapya mnamo tarehe 4 Ogusti 1985 kunako parokia ya Walungu baada ya kusherehekea upadrisho wa wananchi Bahala Okw'Ibale wa parokia ya Ciriri - Bagira, Mbilizi Lwesso wa parokia ya Kadutu na Bulambo Lunanga wa parokia ya Cahi - Ibanda.

Bisimwa L.-B. Tserou.

Je umesikia...?

KWAMBA yule aliyekuwa akijiita kuwa mtumishi wa gazeti Elima ahusikae na matangazo ya biashara (agent publicitaire) amegeuka mwizi ? Kisha kupewa kazi ya kuuza (vendre) na kugawa magazeti katika maofisi mbali mbali ya huko Goma, mwananchi Kafuko Matabaro Baleke Mpaka alianza sasa kugusa nafasi isiyostahili.

Alijiruhusu hata kujimwanga porini (kukimbia) akipeleka baskeli (kinga) la shirika alilokuwa akitumikia (gazeti Elima).

Mpaka sasa, atafutwa nafasi zote lakini lah! Matumaini yetu ni kuona askari walinda amani mikoani (gendarmes) wamnasa na kumtupa nafasi atakapojutia makosa yake na kujisahihisha.

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 n° 282 — Tarehe 31 Ogusti mpaka 6 Septemba 1985

Kiongozi : Mutiri-wa-Bashara

Kisha miaka 15

Barabara Walikale-Masisi imefunguliwa upya

Kisha miezi sita ya kazi ngumu, wakaaji wa mitaa ya Walikale na Masisi walifungua barabara inayounganisha mitaa yao miwili. Barabara hiyo ina kitambo cha kilometri 156. Prezidenti wa Chama jimboni aliye pia liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Mwando Nsimba, alijionea mwenyewe ukweli huo wakati hapo majuzi alitembelea mitaa hiyo tuliotaja hapo juu. Barabara hiyo iliharibika tangu mwaka 1970. Tutakumbuka hapa kuwa huko Walikale wakaaji hulima mpunga, kalanga, muhogo pamoja na ngazi za mchikichi. Udongo wake una madini ya zahabu. Mtaa wa Masisi wajulikana hasa kwa ufugo wa ngombe, mbuzi na kondoo.

Walikale yamka katika usingizi

Alipotembelea Walikale mnamo mwaka 1983, liwali Mwando alivunjwa moyo kwa kutambua kuwa wakaaji wa huko walikuwa wavivu na walevi. Hawakushurulika hata kidogo na kazi za kutengeneza mabarabara ao mlimo. Wanafunzi, walimu na vijana wengine na hata wazee walipendelea hasa zaidi kujielekeza porini kwa kuchimba zahabu.

Kisha miaka miwili mambo yaanza sasa kubadilika. Wakaaji waanza kushurulika na maendeleo ya mtaa wao. Barabara zatengenezwa bila wasiwasi, nyumba zajengwa upya na wanafunzi wajielekeza kwa uwingi shuleni. Kufuatana na jambo hilo, liwali Mwando hakusita kuwapa pongezi wakaaji wa mtaa wa Walikale kwa kuona waliweza kusikia mashauri yake.

Masisi:mipango mipya kwa kupewa udongo.

Huko Walikale kama vile Masisi, wakaaji wamesikia mwito wa Baba wa Taifa na ule wa Liwali wa jimbo la Kivu, na waanza sasa kutia mkazo juu ya maendeleo ya mitaa yao. Lakini kuna bado walakini. Ugonjwa mkali unaowasonga wakaaji wa Masisi ni ule wa kupigania mashamba. Wale matajiri wafanya vyote wawezavyo kwa kuangamiza raia wakiwanyanganya mashamba na kuwafukuza bila huruma yoyote.

Prezidenti wa Chama jimboni aliye pia liwali wa jimbo la Kivu, alitia nukta kwa kumaliza jambo hilo. Aliwakaripia viongozi wa kazi za serikali wanaojiruhusu kuleta mchafuko katika ugawaji wa mashamba. Ni hivi, aliwaelezea kuwa siku hizi hakuna yule atakayepewa shamba huko Masisi, bila sahihi ya pekee ya liwali wa jimbo.

Kaboyi Habimana.

Shahiri

Mateso

Wapi !
Maisha kanitupa
Nyumbani njaa
Kazini magumu
Popote tabu

Niliomba sikupewa
Kosa la nani ?
Ingawa sote twatumika
Mwenye chake na chake

Nilipiga hodi, bure !
Mlango haukufunguliwa
Eti leo si mchezo
Kila mtu kwake

Nilipiga yohe na kulia
Funga kinywa
Maisha ni hivyo
Vumilia ngoja kesho

Niliingia shambani
Kukata na kulima
Wapi ! udongo umechoka
Na ukame umefika

Sasa nifanye je
Nife au...Hapana tafadhali
Jipe tu moyo, utajionea.

Tangolek